BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)

# TAARIFA KWA UMMA

## MABORESHO YA MFUMO WA NAMBA YA UTAMBUZI WA TUZO (AVN)

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linapenda kuutaarifu umma kuwa, linafanya maboresho ya Mfumo wa Namba ya Utambuzi wa Tuzo (Award Verfication Number - AVN) yenye lengo la kuimarisha ufanisi wa mfumo na kuboresha utoaji wa huduma.

Kutokana na maboresho hayo, huduma ya AVN itasitishwa kwa muda wa siku tatu, kuanzia tarehe **14 hadi 16 Julai, 2026,** ili kupisha utekelezaji wa maboresho hayo.

Huduma zinatarajiwa kurejea na kuendelea kutolewa kama kawaida kuanzia **tarehe 17 Julai, 2026.**

Baraza linaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza kutokana na kusitishwa kwa huduma hiyo kwa muda na linawashukuru wadau wote kwa uvumilivu na ushirikiano wao.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko.
**NACTVET**
14 Julai, 2026

NACTVET Makao Makuu, Jengo la Kambarage - Ghorofa ya 7
S. L. P 387, Dodoma | +255 736 310311 | info@nactvet.go.tz | www.nactvet.go.tz